OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

Namba za simu **SHULE YA SEKONDARI UYUMBU,**

Mkuu wa shule: 0757-297258/0622-354368 **S. L. P. 151,**

Makamu mkuu wa shule 0768-234782 **URAMBO.**

19. 05. 2021

KWA: ……..

S. L. P …….

……...

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI UYUMBU MWAKA 2021/2021.**

Uongozi wa shule ya sekondari Uyumbu unayo furaha kubwa kukupongeza kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shule hii. Shule ya sekondari Uyumbu ipo mkoa wa Tabora wilaya ya Urambo tarafa ya Usoke. Shule ipo umbali wa km 50 kutoka Urambo na km 18 kutoka Ussoke. Shule ni ya mchanganyiko na ina tahasusi tano ambazoni **HKL, HGL**, **HGE, PCM na PCB**. Kwa mwanafunzi anayetokea mikoa ya Singinda na Shinyanga shuka kituo cha mabasi Tabora kisha panda gari la kwenda Urambo na shuka Ussoke, kisha panda pikipiki itakayokuleta hadi shuleni. Kwa mwanafunzi anayetoka mkoa wa Kigoma kwa basi au treni shuka Ussoke. Shule itafunguliwa tarehe 12. 07.2021. Wakati wa kupokelewa unatakiwa kuja na mambo yafuatayo:-

i. Fomu ya kujiunga na mahitaji ya shule
ii. Medical examination form
iii. Fomu ya kukubali kujiunga na shule
iv. Historia ya mwanafunzi

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI UYUMBU



1. ADA.

Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs. 70,000/= au Tshs. 35,000/= kwa mhula. Ilipwe benki**, benki ya NMB A/C 51301100031 jina la akaunti ni UYUMBU SEC. SCHOOL REV. COLLECTION A/C. Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye hati ya malipo ya benki (pay in slip) na uiwasilishe shuleni siku ya kuripoti.**

2. MICHANGO MINGINE.

i. Ulinzi, wapishi na vibarua wengine Tshs. 30,000/=
ii. Tahadhari Tshs. 6,000/= (haitarejeshwa)
iii. Ukarabati wa samani Tshs. 15,000/=
iv. Taaluma Tshs. 20,000/=
v. Huduma ya kwanza Tshs. 10,000/=
vi. Nembo ya shule Tshs. 2,000/=
vii. Kitambulisho Tshs. 5,000/=
viii. Mitihani ya majaribio na ujirani mwema Tshs. 20,000/=

Michango yote (i) –(viii) ilipwe benki, benki ya NMB A/C 51306600112 jina la akauti ni UYUMBU SEC. SCHOOL. Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip na uiwasilishe shuleni siku ya kuripoti.

3. SARE YA SHULE.

A. WASICHANA.

i. Sketi mbili (2) linda box ya malinda rangi ya kijivu (grey) ndefu mpaka chini, kitambaa kiwe kizito. Njoo na hela zinapatikana shuleni.
ii. Mashati mawili (2) meupe mikono mirefu
iii. Viatu vyeusi vya kamba kisigoni kifupi jozi mbili (2)
iv. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (2) au zaidi
v. Tai ya kijivu
vi. Hijab/juba jeupe la darasani na juba la kushindia rangi ya njano (kwa anayevaa juba/hijab)
vii. Sketi mbili (2) nyeusi za kushindia
viii. Sweta rangi ya kijivu
ix. T-shirt mbili (2)@12,000/= zinapatikana shuleni

ZINGATIA: Vipodozi vya aina yoyote haviruhusiwi.

Wanafunzi wa kike hawaruhusiwi kusuka nywele.

B. WAVULANA

i. Suruali mbili (2) zenye marinda rangi ya kijivu ISIWE YA KUBANA na kitambaa kiwe kizito

ii. Mashati mawili (2) meupe mikono mirefu
iii. Sweta rangi ya kijivu
iv. Viatu vyeusi jozi mbili (2) zenye kamba
v. Soksi nyeusi mbili (2)
vi. Tai rangi ya kijivu
vii. Mkanda mweusi
viii. Suruali nyeusi ya kushindia. Unashauliwa kuwa suruali zaidi ya moja kuondoa usumbufu.
ix. T-shirt mbili (2)@12,000/= rangi ya njano – zinapatikana shuleni

4. MAHITAJI MENGINE KWA WOTE

i. Shuka mbili (2) blue bahari, mto wa kulalia na neti.
ii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
iii. Godoro 2.5 x 6
iv. Ndoo 2 lita 10 kwa matumizi binafisi
v. Jembe 01
vi. Rimu A_4 mbili (02)
vii. Fyekeo moja (01)
viii. Fagio ya ndani 01
ix. Fagio ya nje chelewa yenye mpini moja (01)
x. Reki moja (01)

5. VIFAA VYA MICHEZO

i. Bukta na T-shirt rangi ya blue (wavulana)
ii. Track suit na T-shirt rangi ya blue (wasichana)
iii. Raba jozi moja
ZINGATIA: T-shirt zisiwe na maandishi ya aina yoyote.

6. VIFAA VYA DARASANI

i. Daftari kubwa angalua 10
ii. Kalamu za wino za kutosha
iii. Kalamu za risasi za kutosha
iv. Kila mwanafunzi anashaurilwa kununua angalau kitabu kimoja kila somo kulingana na tahasusi aliyopangiwa
v. Scientific calculator function 991 kwa wanafunzi wa tahasusi za PCB na PCM
vi. Dissecting tray moja na dissecting kit moja kwa wanafunzi wa PCB
vii. Scientific oxford dictionary

viii. English language dictionary for advanced learners
ix. Kamusi ya Kiswahili-kiingereza na kamusi ya Kiingereza –Kiswahili kwa mada ya TAFSIRI na UKALIMANI

Tafadhari soma kwa makini maagizo/ maekekezo hayo na kuyatekeleza kikamilifu. Vilevile tumeambatanisha fomu A na B nazo zinatakiwa kujazwa kabla ya mwanafunzi kuripoti shule.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule ya sekondari Uyumbu inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya elimu, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – Tamisemi yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kufika shuleni:-

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio kama itakavyokuwa imepangwa (preparation time)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote katika maisha yako ya shule.
f. Kuvaa sare ya shule kikamilifu wakati wote uwapo shule.
g. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
h. Kutunza mali za shule/umma
i. Kuheshima nembo za taifa kama vile wimbo wa taifa, bendera ya Taifa n.k

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

a. Wizi wa aina yoyote ndani au nje ya shule
b. Uasherati na ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, n.k
e. Kupigana au kupiga
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

g. Kudharau bendera ya taifa
h. Kudharau wimbo wa taifa
i. Kubeba mimba na kutoa mimba
j. Kuoa au kuolewa
k. Kugoma au kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule
l. Kukataa adhabu kwa makusudi
m. Kumiliki simu ya mkononi

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO
SHULE YA SEKONDARI UYUMBU
KIAMBATISHO A

Nenda na fomu hii kwa mganga wa serikali akupime na kukujazia

……..
…….
…….
…….

Tarehe ……..

Mganga wa wilaya/mkoa,
S. L. P ……....

MEDICAL CERTIFICATE
Jina la mwanafunzi …….

1. Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona amepatikana na ugonjwa wa …….. na nimemtibu ipasavyo.

2. Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona na ugonjwa hawezi kusoma kwa sababu ya
   …….
   …….

3. Kwa wasichanatu, nimemwona ana mimba/ hana mimba. Tutakayemtilia mashaka tutampeleka hospitali kwa daktari wa hapa wilaya ya Urambo.
4. Afya yake kwa ujumla,

   a. Kifua …….
   b. Macho ……..
   c. Masikio …….
   d. Kilema chochote kitaje …….
   e. Akili ……..
   f. Mkojo ……..

   g. Choo (stool) …….
   h. Mimba …….

Sahihi yam ganga …….. mhuri ……. Tarehe ……..

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

SHULE YA SEKONDARI UYUMBU

S. L. P 151,

URAMBO.

19.05.2021

FOMU B: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

1. Jina la mwanafunzi ……

2. Jina la mzazi/mlezi …….

Mimi ……. Nimekubali kuwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Uyumbu, nimesoma kwa umakini sharia na taratibu zote za shule na kuwa nitazizingatia na kuzifuata wakati wote niwapo shule. Aidha nitajituma kwa bidii katika masomo yangu katika kipindi chote niwapo shuleni. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi …….. tarehe ……..

Mimi ……. Nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……. Naahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mototo na kushirikiana na Uongozi wa shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi ……. Tarehe …….

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

SHULE YA SEKONDARI UYUMBU,

S.L.P 151,

URAMBO.

HISTORIA YA MWANAFUNZI: FOMU (C)

1. Jina la Mwanafunzi: .....
2. Tarehe kamili ya kuzaliwa: .....
3. Jina la Baba: .....
4. Jina la Mama: .....
5. Jina la Mlezi: .....
6. Anuani kamili ya Mzazi/Mlezi: .....
7. Uhusiano wa Mlezi: .....
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi (Mkulima, Mfanyakazi,Mfanyabiashara).....
9. Kama ni Mfanyakazi, kazi yake: .....
10. Kama Mkulima zao muhimu analotegemea: .....
11. Kama Mfanyabiashara, Biashara yake: .....
12. Afya yake (Maelezo kama mwanafunzi anayomatatizo ya kiafya na hivyo anastahili huduma maalum) .....
13. Madhehebu ya dini ya Mwanafunzi: .....
14. Jamaa, Ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya Mzazi/Mlezi;

JINA KAMILI	UHUSIANO	ANUANI YAKE
1)		
2)		
3)		

15. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:

Mimi: .....Nathibitisha kuwa maelezo yaliyotajwa hapo juu ni sahihi.

Anuani ya Mzazi/Mlezi: ..... Tarehe: .....